**TANGAZO**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kuwajulisha watu wote wanaotarajia kufanya **Mtihani wa Kidato cha Sita** (ACSEE) mwaka **2026** kama Watahiniwa wa Kujitegemea kwamba;

1. Kipindi cha usajili kwa Watahiniwa wa Kujitegemea kimeanza tarehe **01/07/2025** hadi **30/09/2025**. Ada ya usajili ni Shilingi **50,000/=**, watakaojisajili kwa **kuchelewa** yaani kuanzia tarehe **01/10/2025** hadi **31/10/2025** watalipa Shilingi **65,000/=** ikiwa ni ada ya kawaida pamoja na faini.

2. Kabla ya kusajiliwa na Mkuu wa Kituo kwenye mtandao, waombaji wanapaswa kwenda kwenye Vituo vya Mitihani kuchukua namba rejea (**reference numbers**) zinazotolewa **bure** na kufanya malipo ya ada kupitia Benki kwa kutumia '**Control Number**'.

3. Ufafanuzi kuhusu utaratibu wa hatua za kufuata katika kutengeneza '**Control Number**' na kujisajili, umetolewa katika tovuti ya Baraza la Mitihani la Tanzania: www.necta.go.tz. Aidha, kwa watahiniwa ambao hawataweza kutumia mfumo huo wapige simu **0738785945** kwa msaada zaidi.

4. Waombaji wote wasisitizwa kuhakikisha wanajisajili mapema kwani mfumo wa usajili utafungwa mara baada ya kipindi cha usajili kukamilika.

Imetolewa na:

**KATIBU MTENDAJI**